

# TAARIFA YA VYOMBO VYA HABARI

---

Ndugu Waandishi wa Habari, tumewaalika hapa kwa sababu tumeona kwamba ni busara katika mazingira tuliyonayo kueleza kwamba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni chombo ambacho hakiwezi kufikia ufanisi unaohitajika katika utendaji wake kama ripoti zake hazitafanyiwa kazi ya kuridhisha na kwa wakati na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Bunge ni taasisi ambazo lazima zielewane na kufanya kazi kwa karibu sana. Kwa maoni yangu ninaamini kuwa, mpaka hivi sasa, nina mahusiano mazuri na yenye tija - siyo tu kati yangu na Spika bali Bunge zima la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, mimi na wakaguzi wangu tumekuwa tukifanya kazi nzuri pamoja na kwa kuaminiana kati yetu na Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Bunge. Huu uhusiano ni wenye umuhimu ili kila moja ya pande hizi mbili [yaani CAG na Bunge] uweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kwa mantiki hiyo ni lazima uenziwe na kudumishwa. Yanayotokea hivi sasa hayatufurahishi, yanatusikitisha.

Majibu yangu katika mahojiano yaliyozua mjadala hayakuwa na nia ya kulidhalilisha Bunge hata kidogo. Maneno kama udhaifu [weaknesses] na mapungufu [deficiencies] ni lugha ya kawaida sana<sup>1</sup> kwa wakaguzi katika kutoa maoni ya utendaji wa mifumo ya taasisi mbalimbali. Ni wazi kwamba watu wengine wanaweza kuchukua tafsiri tofauti ya maneno kama haya. Yametokea malumbano makali na marefu katika nyanja zote za mawasiliano kuhusu rai, nafasi [yaani *positions*] na maamuzi mbalimbali yaliyochukuliwa na viongozi, wanasiasa pamoja na wachangiaji wa kawaida. Mimi binafsi na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi hatuna namna ya kuathiri tafsiri za viongozi, wanasiasa na wachangiaji wa kawaida. Tunachoshauri ni uungwana utawale katika mawasiliano yetu.

Tarehe 15 Januari 2019 nilipokea wito wa kisheria [yaani *summons*] ulionitaka kutokea mbele ya Kamati ya Bunge tarehe 21 Januari 2019. Kwa mantiki hiyo ya kudumisha mahusiano mazuri kati NAOT na Bunge ninayo nia ya kuitikia wito huu hapo tarehe 21 Januari 2019.

Nawashukuru sana kwa kufika na kunisikiliza, Ahsanteni sana.



Prof. Mussa Juma ASSAD  
Controller and Auditor General of the United Republic of Tanzania

---

<sup>1</sup> Kama mumewahi kupitia baadhi ya ripoti zangu mtaona kuwa yametumika mara nyingi sana kukazia maudhui ya hoja za ukaguzi.